

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA KUMI NA NANE

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA PILI
(DAILY SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS)**

28 JANUARI, 2015

MKUTANO WA KUMI NA NANE
YATOKANAYO NA KIKAO CHA PILI
(SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS - SECOND SITTING)
TAREHE 28 JANUARI, 2015

I. DUA:

Dua ilisomwa saa 3.00 asubuhi na Mhe. Spika Anne S. Makinda (Mb) na Kikao kiliendelea.

Makatibu Mezani: 1. Ndg. Lawrence Makigi
2. Ndg. HellenMbeba.

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge aliwasilisha Mezani Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge Uliopita

Toleo Namba 45 – 49 ya Mwaka 2014, naToleo Namba I la Mwaka 2015.

Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali aliwasilisha mezani Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Huduma ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma zilizokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia tarehe 30 Juni, 2013.

Mwenyekiti wa Hesabu za Serikali za Mitaa aliwasilisha mezani Taarifa ya Mwaka ya Kamati kwa Mwaka UlioishiaTarehe 30 Juni, 2013.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aliwasilisha mezani Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati kwa Mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2013.

III. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa:

(i) OFISI YA WAZIRI MKUU:

SWALI NA. 15. Mhe.Peter Msigwa, Mb. (liliulizwa na Mhe. Joseph Selasini)

Nyongeza: (i) Mhe. Joseph Selasini, Mb.
(ii) Mhe. Maria Ibeshi Hewa, Mb.

SWALI NA. 16. Mhe. Goodluck Medeye, Mb (liliulizwa na Mhe. Michael L. Lazier)

Nyongeza: (i) Mhe. Michael LekuleLaizer, Mb.
(ii) Mhe. Joshua Nassari, Mb.

SWALI NA. 17. Mhe. Moshi S. Kakoso, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Moshi S. Kakoso, Mb.
(ii) Mhe. Said A. Arfi, Mb.

(ii) WIZARA YA UCHUKUZI:

SWALI NA. 18. Mhe. Vincent Nyerere, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Aliko Kibona, Mb.
(ii) Mhe. Ester Bulaya, Mb.

(iii) WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

SWALI NA19. Mhe. Letincia Bukwimba, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Letincia Bukwimba, Mb.
(ii) Mhe. Diana Chilolo, Mb.
(iii) Mhe. Assumpta Mshama, Mb.

SWALI NA. 20. Mhe. Ester Nicholas Matiko, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Ester Nicholas Matiko, Mb.
(ii) Mhe. Tundu Antiphas Lissu, Mb.

(iv) WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

SWALI NA. 21. Mhe. Dkt. Augustino Mrema, Mb. (liliulizwa na Mhe. James Mbatia)

Nyongeza: (i) Mhe. James Mbatia, Mb.

SWALI NA. 22. Mhe. Augustino Manyanda Maselle, Mb)

Nyongeza: (i) Mhe. Augustino M. Maselle, Mb.
(ii) Mhe. James Lembeli, Mb.

(v) WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA:

SWALI NA. 23. Mhe. Agripina Buyogera, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Agripina Buyogera, Mb.

(vi) WIZARA YA FEDHA:

SWALI NA. 24. Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu, Mb.

SWALI NA .25. Mhe. Lwanji, Mb. (liliulizwa na Mhe. Selemani Jafo)

Nyongeza: (i) Mhe. Selemani Jafo, Mb.

(vii) WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

SWALI NA. 26. Mhe. Maria Ibeshi Hewa, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Maria Ibeshi Hewa, Mb.

SWALI NA. 27. Mhe. Amina Makilagi, Mb (liliulizwa na Mhe. Felista Bura)

Nyongeza: (i) Mhe. Felista Bura, Mb.

(viii) WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

SWALI NA. 28. Mhe. Clara Diana Mwatuka, Mb.

Nyongeza: (i) Mhe. Clara Mwatuka, Mb.

(X) WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

SWALI NA. 29 Mhe. Juma Abdallah Njwayo, Mb.

Nyongeza: Mhe. Juma Abdallah Njwayo, Mb.

V. MATANGAZO:

- (a) Wageni wote waliokuwepo katika gallery ya Spika na gallery ya Maafisa walitambulishwa.
- (b) Kamati zifuatazo zilitakiwa kukutana saa 7.00 mchana katika kumbi mbalimbali
 - (i) Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala
 - (ii) Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira
 - (iii) Kamati ya Miundombinu
 - (iv) Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

VI. HOJA YA DHARURA:

Mhe. James Mbatia, Mb alisimama chini ya Kanuni ya (47) na kutoa Hoja ya dharura akiliomba Bunge kusitisha Shughuli zilizokuwa zinaendelea ili kujadili jambo la dharura kufuatia kitendo kilichotokea jana tarehe 2/01/2015 jijini Dar es Salaam, kwa Polisi kumkamata Mwenyekiti wa Cuf. Prof. Ibrahim Lipumba na wafuasi 32 wa Chama cha CUF na kuwapiga kwa kilichodaiwa kuwa walifanya Maandamano bila kibali.

Alieleza kuwa awali Chama hicho kilipewa kibali cha kufanya Maandamano na muda mfupi kabla ya kuanza Polisi walisitisha Maandamano hayo kwa maelezo kuwa wamepewa maagizo kutoka juu, ambapo kutokana na uamuzi huo wa Polisi Prof. Lipumba aliamua kuelekea eneo walilopanga kuandamana ili kutoa taarifa kwa wafuasi wake ndipo Polisi walipovamia msafara wake na kutumia nguvu kubwa kwa kuwapiga na kuwakamata pamoja na kurusha mabomu yaliyowadhuru watu wasiohusika wakiwemo watoto wadogo.

Alieleza kuwa kwa kuwa vitendo kama hivi vimekuwa vikijitokeza mara kwa mara bila kuchukuliwa hatua stahiki kwa kutoa mfano kuwa tarehe 9 na 10/7/2013 Vyama vyote vilivyotoka chini ya TCD vilifanya kikao na Mhe. Rais na kuongea juu ya vitendo hivi lakini vimekuwa vikijirudia, na kwamba kwa kumdhalilisha Prof. Lipumba ambaye ni Kiongozi Mkuu wa Chama cha CUF, kinachounda Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar ni kitendo ambacho hakistahiki kufumbiwa

macho hivyo, Bunge lijadili na Serikali itoe majibu hilo agizo lilikuwa la nani na lilitolewa kwa malengo gani.

VII. UAMUZI WA MWENYEKITI:

Mhe. Spika alitoa maelezo kuwa kwa kuwa jambo hilo ni kubwa aliagiza Serikali kutoa maelezo juu ya kilichotokea kesho yake tarehe 29/01/2015 na baadaye Bunge lijadili kwa upana juu ya jambo hilo.

Baada ya uamuzi huo wa Spika, Wabunge wote wa Upinzani waliokuwa Bungeni walisimama na kuanza kuongea bila utaratibu kila mmoja akisema maneno yake kwa sauti hali iliyopelekea fujo Bungeni na Bunge kushindwa kuendelea na Shughuli nyingine.

VIII. KUSITISHA BUNGE:

Kutona na fujo hizo, Mhe.Spika alilisitisha Bunge saa 5.30 asubuhi mpaka saa 10 jioni.

IX. BUNGE KUREJEA:

Bunge lilirejea saa 10.00 jioni likiongozwa na Mhe. Spika na alianza kwa kuwaeleza Wabunge kuwa, baada ya kuahirisha Bunge asubuhi Kamati ya Uongozi ya Bunge ilikutana na kujadiliana kwa kina juu ya jambo lililotokea asubuhi na kukubaliana kwamba, Bunge litakaporejea jioni kusiwe na shughuli yoyote isipokuwa Spika aliahirishe mpaka kesho yake saa 3.00 asubuhi ambapo baada ya kipindi cha Maswali watakuwa na mjadala juu ya hoja ya dharura iliyotolewa na Mhe. James Francis Mbatia.

X. KUAHIRISHA BUNGE:

Mhe.Spika aliahirisha Bunge saa 10.07 jioni hadi kesho yake saa 3.00 asubuhi.

**DODOMA
28 JANUARI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**